# MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF)

## KUHUSU MFUKO NA HUDUMA ZINAZOTOLEWA

# Yaliyomo

- Kuanzishwa kwa Mfuko wa PSSSF
- Wanachama wa Mfuko
- Uandikishaji wa Waajiri na Wanachama
- Uwasilishaji wa Michango
- Jukumu la Mwajiri, mwanachama na Mfuko
- Ulipaji wa mafao
- Manufaa ya muunganiko wa Mifuko

# Kuanzishwa kwa PSSSF

- **Tarehe 20 Oktoba, 2017 Serikali ilipitisha uamuzi wa:-**
  - Kuunganisha Mifuko ya Pensheni ya PSPF, LAPF, GEPF na PPF na kuunda mfuko mmoja wa PSSSF kwa ajili ya Watumishi wa Umma na;
  - Kuufanyia marekebisho Mfuko wa NSSF ili uwe Mfuko mahsusi kwa ajili ya wafanyakazi wa Sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Kuanzishwa kwa PSSSF inaendelea…

- Sheria inayoanzisha Mfuko huu ilipitishwa na Bunge tarehe 31/01/2018 na
- Kusainiwa na Mhe Rais tarehe 8/2/2018. hii ni Sheria Na 2 ya mwaka 2018.
- Utekelezaji wa Sheria ilitangazwa kwenye gazeti la Serikali kuwa tarehe 1/8/2018

# Wanachama wa PSSSF

- Wanachama wote wa iliyokuwa mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF
- Watumishi wote wa Umma na taasisi zake watakaoajiriwa kuanzia tarehe 1/8/2018
- Watumishi wote wa taasisi na makampuni ambayo Serikali au taasisi zake zinamiliki zaidi ya asilimia 30% ya hisa

# Wanachama wa Mfuko …….

- **Kwa sasa hakuna ushindani tena hivyo**:
  - Kila mwajiri (Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, taasisi na wakala wa Serikali) watapaswa kuwaandikisha watumishi wao PSSSF mara tu wanapowaajiri na kuwajazisha fomu mbalimbali za ajira *(Waajiri watapewa fomu hizo)*
  - Baada ya kuwaandikisha watatoa taarifa kwenye Mfuko kwa ajili ya kukamilisha fomu hizo na kuwaandikisha kwenye mfumo wa PSSSF

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Wastaafu

- Wastaafu wote walikuwa wanalipwa pensheni zao na mifuko ya PSPF, PPF, LAPF na GEPF kuanzia tarehe 1/8/2018 walitambulika kama wastaafu wa PSSSF na pensheni zao zitaendelea kulipwa na PSSSF.
- Wastaafu wote watakaoendelea kustaafu kuanzia tarehe 1/8/2018 watakuwa wastaafu wa PSSSF na watalipwa pensheni zao na Mfuko.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Uandikishaji wa Waajiri

- Waajiri wote waolikuwa waajiri wachangiaji wa LAPF, PSPF, PPF na GEPF watatambulika kuwa waajiri wachangiaji wa PSSSF
- Waajiri watapewa  hati mpya ya uandikishaji itakayowekwa mahali panapoonekana katika ofisi yake.

# Uandikishaji wa Wanachama

- Wanachama wote wa PSSSF watatambulika kwa namba zao za uandikishaji walizokuwa nazo
- **LAKINI** Kuanzia tarehe 1/8/2018 wanachama wote wa Mfuko watatambuliwa kwa namba ya utaifa *(National Identification Number)*
- Hivyo wanachama wote wanatarajiwa ifikapo 30/6/2019 watakuwa na kitambulisho cha Taifa.

# Uwasilishaji wa Michango

- Watumshi wa Umma wataendelea kuchangia kiasi cha 5% ya mishahara yao kila mwezi na
- Mwajiri atachangia 15% ya mshahara wa mtumishi na atawajibika kuwasilisha PSSSF
  - Ndani ya mwezi wa michango hiyo au
  - Ndani ya mwezi unaofuata mwezi wa michango hiyo

# Uwasilishaji wa Michango

- Kipindi hicho kikipita mwajiri atatakiwa kulipa michango ya ziada (adhabu) kwa kiwango cha 1.5% kwa kila mwezi ambao mchango imechelewa.

# Jukumu la Kuhakikisha Michango Inalipwa

- Makundi matatu yanawajibika kuhakikisha michango inawasilishwa
  - **(i) Mwajiri** anapaswa kumkata mtumishi toka kwenye *payroll*
  - Kujumuisha michango ya mwajiri na kuwasilisha 20% kwenye Mfuko

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Jukumu la Kuhakikisha Michango Inalipwa

- **(ii) Mwanachama** wa Mfuko anapaswa kujihakikishia kupitia *salary slip* yake kuwa amekatwa toka kwenye mshahara wake mchango wa PSSSF.
- **(iii) PSSSF** inawajibika kisheria kufuatilia michango na kuhakikisha inalipwa. Ina uwezo pia wa kumshitaki mwajiri ambaye hajawasilisha michango

# Kumbukumbu za Wanachama na Michango

- Mwanachama anaweza kupata taarifa zake binafsi na michango wakati wowote atakapoomba toka kwenye ofisi za PSSSF
- Aidha, anaweza kuzipata kupitia tovuti ya Mfuko ambayo ni www.psssf.go.tz

# PSSSF Inatoa Mafao Yafuatayo

- Pensheni ya Uzee
- Pensheni ya Ulemavu
- Pensheni ya Warithi
- Mafao ya Ugonjwa
- Mafao ya Kukosa ajira
- Mafao ya uzazi

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Pensheni ya Uzee

- Sifa za kupata pensheni ya Uzee:
  - Uchangiaji usiopungua miezi 180 au miaka 15
  - Umri wa kustaafu
    - Kwa hiari au
    - Kwa lazima (miaka 50, 55, 60 au 65 kuendana na masharti ya ajira ya mstaafu)

# Mfano

- Kwa Polisi
  - Vyeo vyote hadi cheo cha Inspekta wa polisi umri wa kustaafu kwa lazima ni miaka 55
  - Maafisa wa vyeo juu ya Inspekta wanastaafu kwa lazima wakifika miaka 60

# Mfano…..

- **Kwa Askari Magereza**
  - Warders au Wardress wanastaafu wakifika miaka 50
  - Vyeo vinavyofuata hadi cheo cha RSM wanastaafu wanapofikia miaka 55
  - Maafisa wa vyeo juu ya RSM wanastaafu kwa lazima wanapofika miaka 60

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Kikokotoo cha Pensheni ya Uzee

- Wanachama wote wa PSPF, LAPF na GEPF waliokuwa na umri wa miaka 55 au zaidi ilipofika tarehe 1/8/2018 watakapostaafu watalipwa mafao kwa kutumia vikokotoo viwili. (cha zamani na kikokotoo kipya):-
  - (i) Pensheni ya mwaka kwa kikokotoo cha zamani kwa utumishi wote hadi tarehe 31/7/2018

**Pensheni =1/540 X Miezi ya Utumishi X Mshahara wa mwisho kwa mwaka**

# Kikokotoo cha Pensheni ya Uzee…….

- (ii) Pensheni ya mwaka kwa kikokotoo kipya kwa utumishi wote kuanzia tarehe 1/8/2018 hadi umri wa kustaafu ni

**Pensheni = 1/580 X Miezi ya Utumishi X Wastani wa mishahara ya miaka mitatu (APE)**

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Malipo ya Mkupuo

**(Pensheni kwa kikokotoo cha zamani) x 0.25 x 15.5**

Jumlisha

- **(Pensheni kwa kikokotoo kipya) x 0.25 x 12.5**

# Malipo ya pensheni ya Kila Mwezi

**MP1 = (Pensheni kwa kikokotoo cha zamani) x 0.75**

**x 1/12**

Jumlisha

**MP2 = (Pensheni kwa kikokotoo kipya) x 0.75 x 1/12**

- **Hivyo basi Pensheni ya mwezi= MP1 + MP2**

# Mfano

- Mwanachama "A" tarehe 1/8/2018 alikuwa na miaka 56
- Ana miaka 4 kufikia miaka 60
- Mshahara wa mwisho ni = Sh. 1,268,000/=
- Aliajiriwa tarehe 1/7/1980
- Wastani wa mishahara ya miaka mitatu (APE) = Sh. 1,178,000/=

# Mfano……….

**Pensheni ya mwaka kwa kipindi kabla ya 1/8/2018** ni

=(1/540 x 457 x 1,268,000 x 12)

= **TZS 12,877,244.44**

**Malipo ya Mkupuo** = Pensheni ya Mwaka x 0.25 x15.5

= **TZS 49,899,322.22**

Pensheni ya mwezi = (Annual Pension x 0.75)/12

= TZS 804,827.78

# Mfano..........

**Pensheni ya mwaka kwa kipindi Baada ya 1/8/2018** ni

=(1/580 x 505 x 1,178,000 x 12)

**= TZS 12,308,069**

**Malipo ya Mkupuo = Pensheni ya Mwaka x 0.25 x12.5**

**= TZS 38,462,715.52**

**Pensheni ya Mwezi = (38,462,715.52 x 0.25 x 12.5x 0.75)/12**

**= TZS 600,979.93**

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Mfano...

**Malipo ya Mkupuo kwa kipidi cha miaka  mine (4) baada ya 1/8/2018**

**= 48/505*38,462,715.5**

**= TZS 3,655,862.06**

**Pensheni ya kila mwezi =** (48/505 x0.75x 12,308,068.96)/12

**= TZS 73,117.24**

- **Mkupuo kwa kipindi hadi miaka 60** =

=TZS 49,899,822.22  + TZS  3,655,862.06

**= TZS 53,555,684.28**

# Mfano..........

- MP1=Pensheni ya kila mwezi = 12,877,244.44 x 0.75 x 1/12

  = TZS 804,827.78

- MP2=Pensheni ya kila mwezi = 1,169,875.86 x 0.75 x 1/12

  = TZS 73,117.24

- **Jumla ya Pensheni ya mwezi = MP1 + MP2**

  **=TZS 877,945.02**

# Kuongezeka kwa Pensheni ya Mwezi

- Pensheni ya kila mwezi itaongezeka kila baada ya miaka 3 kuendana na mfumuko wa bei:-
  - Kama mfumuko wa bei uko kati ya 1% hadi 10% nyongeza ya pensheni itaongezeka kwa nusu ya kiwango cha mfumuko wa bei.
  - Mfumuko ukiwa zaidi ya 10% nyongeza itakuwa 5% ya pensheni.
  - Kama mfumuko wa bei uko chini ya 1% hakutakuwa na nyongeza

# Punguzo Katika Pensheni

- Mwanachama akistaafu kwa hiari, pensheni yake ya kila mwezi itapunguzwa kwa kiwango cha 0.3% kwa kila mwezi aliowahi kuchukua pensheni

- Pensheni ya kila mwezi haitakuwa pungufu ya 40% ya kima cha chini cha mshahara wa sekta husika

- Pensheni ya kila mwezi itaanza kutolewa mwezi unaofuata mwezi wa kustaafu.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Pensheni Iliyoahirishwa (Deferred Pension)

- Pensheni ya kila mwezi itaahirishwa endapo Mwanachama:-
    - Amestaafishwa kwa manufaa ya umma
    - Amepunguzwa kazi (Retrenched)
    - Amestaafishwa kwa manufaa ya Umma
    - Ameteuliwa kuingia kwenye nafasi ya kisiasa yenye utaratibu mwingine wa mafao.
    - Amekosa kazi kwa kufungwa shughuli za mwajiri
- Akiwa amechangia Mfuko kwa miaka 15 au zaidi.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Pensheni Iliyoahirishwa (Deferred Pension)….

- Pensheni iliyoahirishwa itaanza kutolewa mwanachama atakapofikisha umri wa kustaafu kwa hiari
- Malipo ya mkupuo hulipwa mara tu anapostafishwa
- Wanachama watakaotoka kazini wakiwa na uchangiaji chini ya miaka 15 watalipwa malipo ya mkupuo (Special lump sum) ambayo ni michango yake, ya mwajiri pamoja na riba.

# Pensheni ya Ulemavu

❑ **Pensheni ya Ulemavu italipwa kwa mwanachama :-**

- Aliyeachishwa kazi kutokana na ugonjwa ambao hauhusiani na kazi.
- Ambaye yuko chini ya umri wa kustaafu kwa hiari
- Amechangia kwenye mfuko kwa miezi 36 na kati ya hiyo 12 ni kabla kuachishwa kwa ugonjwa.

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Pensheni ya Ulemavu

- Kanuni ya kulipa mafao ya uzee itatumika kukokotoa pensheni ya ulemavu
- Pensheni ya kila mwezi haitakuwa chini ya 30% ya mshahara wake.
- Pensheni hiyo itakuwa inaongezeka pia kuendana na mfumuko wa bei
- Italipwa hadi mwanachama atakapofariki

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Pensheni ya Warithi

- Endapo mwanachama amefariki akiwa amechangia Mfuko kwa miaka 15 au zaidi
- Mfuko utaandaa mafao yafuatayo kwa ajili ya wategemezi:
  - Fao la kifo (mkupuo) na
  - Pensheni ya warithi
- Kama hakuchangia kwa kipindi chini ya miaka 15 wategemezi watalipwa malipo ya mkupuo

# Malipo ya Mkupuo (Death Gratuity)

- Endapo mwanachama aliyefariki ameacha mke/mume na watoto:-
  - Mjane au mgane atapata 40% ya malipo ya mkupuo
  - Watoto wanapata = 60%

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Malipo ya Mkupuo (Death Gratuity)..........

- Endapo hakuna watoto  mjane/mgane atapata 100%
- Endapo wamebaki watoto pekee  watalipwa 100%
- Kama watoto waliobaki wanasoma
  1. Kiasi cha malipo ya Mkupuo kitagawanywa  na nusu itabaki ofisini kwa ajili ya kugharamia elimu
  2. Kiasi kilichobaki kitagawanywa

# Pensheni ya Warithi

- Pensheni ya warithi inalipwa pale ambapo mwanachama aliyefariki alichangia Mfuko kwa miezi 180 au zaidi.
  - Pensheni ya kila mwezi itapatiakna kwa kikokotoo kama cha mafao ya kustaafu kwa uzee.

# Pensheni ya Warithi……………………..

- Mgawanyo wa pensheni ya kila mwezi:-
  - Endapo mjane au mgane aliyeachwa ana miaka 45 au zaidi atalipwa pensheni maisha yake yote au hadi atakapooa au kuolewa
  - Endapo mjane au mgane aliyebaki  ana umri chini ya miaka 45 lakini ana watoto walio na umri chini ya miaka 15 atapata pensheni kwa maisha yake yote

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Pensheni ya Warithi……………………..

- Watoto walio chini ya miaka 21 lakini wanasoma watapata pensheni
- Endapo marehemu hakuacha mjane/mgane au watoto basi wazazi walikuwa wanamtegemea watapata pensheni ya mwezi hadi watakapofariki dunia.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Kukoma kwa Pensheni

- Endapo mstaafu amefariki dunia waliobaki watalipwa mkupuo sawa na pensheni ya marehemu kwa miezi 36.
- Pensheni ya watoto itakoma watakapofikia miezi 21 kama wanasoma au miaka 18 kama hawasomi
- Mjane au mgane atakapoolewa au kuoa tena

# Kujumuisha Vipindi vya Uchangiaji

- Endapo mwanachana atakuwa amechangia mifuko zaidi ya mmoja utaratibu wa kujumuisha vipi vya uchangiaji utatumika katika kulipa mafao.

# Fao la Kukosa Ajira

- Fao hili linatolewa kwa wanachama wa PSSSF ambao wameachishwa kazi bila hiari yao
- Kiasi kitakacholipwa ni 33.3% pensheni ya kila mwezi
- Inalipwa kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia tarehe ya kukosa ajira

# Fao la Kukosa Ajira…………..

- Ikipita miezi 18 baada ya miezi sita ya mwanzo kupita, mwanachama anaweza kuomba kuhamisha michango yake kwenda kwenye mfumo wa hiari.
- Michango pamoja na riba vitahamishwa baada ya kuondoa fao la kokosa kazi lililolipwa awali

# Fao la kukosa Ajira…..

- Mwanachama aliyehamisha michango yake kwenda kwenye mfumo wa hiari anaweza kuendelea kuchangia katikamfumo huo.
- Mwanachama aliyekosa kazi akiwa hajachangia mfuko kwa miezi 18 atalipwa nusu ya michango yake mara moja tu.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Fao la kukosa Ajira…..

- Mwanachama aliyepata fao la kukosa kazi na ambaye hakuhamisha michango yake kwenda kwenye mfumo wa hiari
    - Kipindi chake chote cha uchangiaji kitatumika katika kumlipa mafao ya uzee atakapofikisha umri wa kustaafu

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Fao la Ugonjwa

- Fao hili linatolewa kwa mwanachama ambaye
  - amepata ugonjwa ai ajali uliomsababishia kupewa likizo
  - Ugonjwa au ajali aliopata haihusiani na kazi alokuwa anafanya
  - Analipwa nusu mshahara kwa kutokuwa kazini
  - Ana umri chini ya umri wa kustaafu kwa hiari
  - Amechangia Mfuko kwa miezi 36 au zaidi

# Fao la Ugonjwa

- Fao la ugonjwa litaanza kulipwa baada ya siku 63 za likizo ya ugonjwa
- Litalipwa kwa miezi mitatu tu.
- Kiwango cha malipo ni 40% ya mshahara wa mwanachama husika.

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Mkupuo Maalum kwa wanaohama Nchi

- Mwanachama anayehama nchi kwenda nchi nyingine na ambaye hana mpango wa kurudi ataweza kulipwa mkupuo maalum ambao ni
  - Michango pamoja na riba ya uwekezaji

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Thamana kwa Mikopo ya Ujenzi

- Mwanachama anaweza kukopa toka benki kinacholingana na nusu ya mafao yake wakati anafanya maombi hayo.
- Mfuko utaingia makubaliano na benki kwa lengo la kuhakikisha riba inakuwa ya chini

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Masharti ya Mkopo

- Lazima mwombaji awe mwanachama wa PSSSF
- Amechangia kwa kipindi kisichopungua miaka 10
- Urejeshaji wa mkopo huo hautazidi kipindi chake cha utumishi kabla ya kustaafu
- Awe mtanzania

PSSSF Public Service Social Security Fund

# Manufaa ya kuanzishwa kwa PSSSF

- Malipo makubwa zaidi ya pensheni ya kila mwezi hadi kifo
- Pensheni kuongezwa kila baada ya miaka mitatu kuendana na mfumuko wa bei
- Mjane/mgane kulipwa pensheni maisha yake yote
- Kuanzishwa kwa fao la kukosa kazi
- Kuanzishwa kwa ugonjwa
- Mafao kwa wategemezi ya miezi 36 baada ya mstaafu kufariki dunia

# Manufaa ya kuanzishwa kwa PSSSF…….

- Pensheni hadi kifo kwa wazazi wa mwanachama aliyefariki dunia akiwa hajaacha mjane/mgane au watoto.
- Malipo ya mkupuo makubwa kuliko kiasi cha michango kilichochagwa na mwanachama pamoja na mwajiri

PSSSF
Public Service
Social Security Fund

# Manufaa ya kuanzishwa kwa PSSSF………..

- Huduma bora zaidi
  - Ofisi kila mkoa
  - Malipo ya mafao ya muda mfupi kwenye mkoa
  - Pensheni kulipwa kila tarehe 25 ya mwezi
  - Malipo ya mafao moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mwanachama
  - Mafao ya kustaafu kabla au ifikapo tarehe ya kustaafu (maombi kuwasilishwa miezi 6 kabla ya tarehe ya kustaafu)

# ASANTENI